JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Bodi ya Usajili wa Wathamini**

**Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi,**
**Chuo Kikuu cha Dodoma, CIVE Ghorofa 1,**
**S. L. P. 325, Dodoma, Tanzania**
**Simu Na: +255 733542654 email. Registrar@vrb.go.tz**

**Kumb. Na. AB.26/36/01/44** **Tarehe 20 Februari, 2025.**

# TANGAZO KWA UMMA

## MAFUNZO KWA AJILI YA KUWEZESHA WATHAMINI KUSAJILIWA KATIKA KUNDI LA USAJILI KAMILI NCHINI

Bodi ya Usajili wa Wathamini inapenda kuwatangazia Wathamini wote nchini kwamba inategemea kuendesha mafunzo kwa ajili ya kuwezesha Wathamini kusajiliwa katika kundi la Usajili Kamili, kama ilivyoainishwa katika Kifungu namba 28 (c) cha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini,Sura ya 318.

2. Udahili utahusisha mafunzo na mitihani kwa Wathamini wote waliomaliza shahada ya kwanza si chini ya miaka mitatu iliyopita, awe amesajiliwa katika kundi la Wathamini wa Awali (Provisionally Registered Valuer), awe amewasilisha orodha ya kazi za uthamini alizokwisha fanya (logbook) na amelipia gharama husika.

3. Gharama za ushiriki wa mafunzo haya ni Tshs 200,000/= kwa kila hatua, mafunzo yataendeshwa kwa hatua zote tatu za mitihani kama ilivyoainishwa katika Kanuni ndogo namba 9 (1) (b) Kanuni ndogo za Mitihani na Mafunzo, 2020 na marekebisho yake.

4. Usajili wa Wathamini unafanyika katika Ofisi za Bodi, fomu zinapatika katika tovuti ya Bodi (www.vrb.go.tz), Fomu hizo zitapokelewa kwa njia ya barua pepe registrar@vrb.go.tz rasmi kuanzia tarehe ya tangazo hili.

***Bodi inawakumbusha ni kosa la jinai kufanya kazi za uthamini nchini bila ya kusajiliwa na Bodi.***

**MSAJILI**